



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MAELEZO KUHUSU ZOEZI LA KUCHUKUA NA KUREJESHA FOMU ZA MAOMBI YA UTEUZI WA KUGOMBEA NAFASI ZA UONGOZI KATIKA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2019

Kwa mujibu wa Kanuni ya 16(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Tangazo la Serikali Na. 371, Kanuni ya 17(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Tangazo la Serikali Na. 372, Kanuni ya 17(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Tangazo la Serikali Na. 373 na Kanuni ya 17(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Tangazo la Serikali Na. 374, Fomu za maombi ya uteuzi wa kugombea nafasi za Uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 zimeanza kutolewa na kurejeshwa kuanzia tarehe 29 Oktoba, 2019 na zitaendelea kutolewa na kurejeshwa hadi tarehe 4 Novemba, 2019.

Kiujumla mpaka sasa **zoezi hili linaendelea vizuri** katika maeneo mengi kulingana na taarifa tulizopokea, **isipokuwa** kumejitokeza malalamiko katika baadhi ya maeneo kutoka kwa baadhi ya Vyama vya Siasa kuhusu zoezi la uchukuaji na urejeshaji wa Fomu. Malalamiko mengi yalilenga suala la Mihuri, kutokuwepo Vituoni baadhi ya wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, baadhi ya Wasimamizi kutofungua kwa wakati Vituo vya kuchukulia fomu pamoja na masuala mengine ya kikanuni.


Kutokana na malalamiko hayo, Mamlaka ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa inaelekeza na kuisisitiza kwamba uchukuaji na urejeshaji wa Fomu za maombi ya uteuzi wa kugombea nafasi za uongozi uzingatie Kanuni za Uchaguzi na Miongozo iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizo. Hivyo, Wasimamizi/Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, Vyama vya Siasa na Wadau wengine wa Uchaguzi wanapaswa kuzingatia masharti na Miongozo iliyotolewa kuhusiana na uchukuaji na urejeshaji wa Fomu.

Kwa kuzingatia maelekezo haya ya kiujumla hatutarajii suala lolote la kutozingatiwa kwa Kanuni za Uchaguzi kutoka kwa Wasimamizi/Wasimamizi wasaidizi, Vyama vya Siasa na Wadau mbalimbali. Maelezo haya yamejumuisha hoja mbalimbali zilizowasilisha Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Mamlaka ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa inaendelea kufuatilia kwa karibu zoezi hili la utoaji na urejeshaji wa Fomu. Nitoe wito kwa Wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za Uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe **24 Novemba, 2019**.

MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI AFRIKA

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.



Selemani S. Jafo (Mb.)
WAZIRI WA NCHI
OFISI YA RAIS - TAMISEMI

30 OKTOBA, 2019